TANZANIA BREWERIES LIMITED

MKUTANO MKUU WA 45 WA WANAHISA

KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA AROBAINI NA TANO WA WANAHISA WA KAMPUNI YA TANZANIA BREWERIES LIMITED ULIOFANYIKA UKUMBI WA RUAHA KATIKA KITUO CHA MIKUTANO CHA JULIUS NYERERE, DAR ES SALAAM TAREHE 23 MWEZI AGOSTI, 2018, SAA NNE NA NUSU ASUBUHI

WALIOKUWEPO

HON. C. D. MSUYA	Mwenyekiti
MR. R. JARRIN	Mwakilishi wa ABINBEV AFRICA BV
MR. L. MUSUSA	Mjumbe wa Bodi
WANAHISA WENGINE	Majina yao yapo katika 'Kiambatisho A'

WENGINE WALIOHUDHURIA

MR. HURUMA NTAHENA :	Katibu

WALIOALIKWA KUTOKANA NA MAJUKUMU YAO YA KAZI

BW.B. ZAMBRANO	Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara TBL
BI.A. WALTER	Msaidizi wa Mkurugenzi Mkuu wa TBL
BI.Z. TENGA	Meneja Mawasiliano wa TBL

KUMB. NAMBA 1/2018 : KUSOMA TAARIFA YA MKUTANO

1.1. Katibu alisoma taarifa ya Mkutano Mkuu wa 45 wa Wanahisa wa kampuni ya Tanzania Breweries Limited, uliofanyika kwenye ukumbi wa Ruaha - Mwalimu Nyerere Convention Centre, Dar es Salaam, kuanzia saa nne na nusu asubuhi.

KUMB. NAMBA 2/2018 : AKIDI YA MKUTANO

2.1. Katibu, alithibitisha kupokea hati ya uwakilishi kutoka AB InBev Africa B. V, kumchagua, Bw. R. Jarrin, kuwakilisha AB InBev Africa B.V katika mkutano huo mkuu wa 45 wa Wanahisa.

2.2. Katibu alithibitisha kuwa kwa mujibu wa kanuni ya 62 ya mwongozo wa kampuni ya Tanzania Breweries Limited, akidi ya Mkutano Mkuu wa Wanahisa ni wanahisa wasiopungua wawili wenye hisa asilimia 50% au zaidi, na mmoja wao anapaswa kuwakilisha kampuni ya AB InBev Africa B.V (zamani SABMiller Africa B.V.).

2.3. Katibu alithibitisha kuwa akidi ya Mkutano ilitimia.

KUMB.. NAMBA 3/2018: AGENDA ZA MKUTANO

3.1. Ajenda zilizowasilishwa ni:

(i) Taarifa ya kuitishwa Mkutano

(ii) Kupitia na kuthibitisha ajenda za Mkutano Mkuu uliopita.

(iii) Yatokanayo na ajenda za Mkutano Mkuu uliopita

(iv) Kupitia taarifa za hesabu za kampuni na Wakurugenzi katika kipindi kilichoishia tarehe 31, Desemba, 2017.

(v) Kuthibitisha gawio lililolipwa katika mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2017.

(vi) Kuchagua kampuni ya PricewaterhouseCoopers kama wakaguzi wa mahesabu ya kampuni katika kipindi kinachoishia tarehe 31, Desemba, 2018.

(vii) Masuala mengineyo

3.2. Ajenda zilipitishwa kwa majadiliano.

KUMB. NAMBA 4/2018: KUPITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU ULIOPITA

4.1. Kumbukumbu za za Mkutano Mkuu uliopita zilisomwa na kuthibitisha kuwa kumbukumbu sahihi za mkutano huo.

KUMB. NAMBA 5/2018: YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU ULIOPITA

5.1. Wajumbe walijulishwa kuwa Baraza la Ushindani (FTC) lilikuwa bado halijatoa uamuzi wa rufaa iliyowasilishwa kupinga uamuzi uliotolewa na Tume ya Ushindani, uliotaka TBL kuuza hisa zake katika kampuni la Tanzania Distilleries Limited (TDL) (65%).

5.2. Iliripotiwa kuwa ongezeko la mtaji na hisa za TBL lilisajiliwa. Hisa mpya 127,600 zenye thamani ya Tsh. 100 kila moja zilisajiliwa katika rejista ya TBL, katika Soko la Hisa la Dar es alaam (DSE) na rejista kuu iliyounganishwa ilipelekwa katika Soko la Hisa.

5.3. Wajumbe walifahamishwa juu ya kuteuliwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Profesa. Elisante Ole Gabriel na Naibu Katibu wa Wizara ya Fedha na Mipango kwenye Bodi ya Wakurugenzi, wakiwa wanaiwakilisha Serikali. Hata hivyo Profesa Elisante, alihamishiwa Wizara ya Kilimo na Dk. Khatibu.M. Kazungu, alikuwa Dodoma hivyo kushindwa kufanya mkutano kati yao na Wajumbe wenye hisa chache kama tulivyokubaliana katika mkutano uliopita.

5.4. Mwenyekiti aliwahakikishia wajumbe kuwa Bodi kwa kushirikiana na Uongozi itapitia mapendekezo yao na kuyawasilisha kwa wajumbe wa Bodi wanaoiwakilisha Serikali ili kuhakikisha kuwa wanahisa wanapata fursa ya kukutana na kubadilishana mawazo na wawakilishi wao katika Bodi.

5.5. Wajumbe walipokea taarifa hiyo

KUMB. NAMBA 6/2018: KUTHIBITISHA TAARIFA ZA FEDHA ZA MWAKA NA TAARIFA ZA WAKURUGENZI

6.1. Mwenyekiti aliwakaribisha wanahisa katika Mkutano Mkuu wa 45. Alisema ripoti ya mahesabu iliyotolewa ni ya kipindi cha miezi tisa (Aprili hadi Desemba) hadi Desemba 31, 2017. Kutokana na kuthibitishwa kubadili kipindi cha kutoa ripoti za mwaka katika mkutano mkuu uliopita. Katika kipindi hiki mauzo yaliongezeka na kufikia hectolita milioni 3.3 ambayo ni ongezeko la asilimia 24, mapato yaliongezeka kwa asilimia 9 na ukuaji wa faida ya uendeshaji uliongezeka kwa asilimia 16 kulinganisha na kipindi cha miezi 9 cha mwaka uliopita. Kutokana na hali hiyo kibiashara iliwezesha kutolewa gawio la shilingi 770/- kwa kila hisa ikiwa ni ongezeko la asilimia 120 kulinganisha na mwaka uliopita.

6.2. Alisema kampuni imekabiliana na changamoto mbalimbali katika mifumo na uendeshaji katika kipindi cha mpito cha mabadiliko kuendana na mifumo ya kampuni ya ABInBev inayoendesha shughuli za kampuni kwa sasa. Licha ya changamoto hizo, kampuni ilikua kwa asilimia 30 na kuongeza mauzo ya bia kwa asilimia 8,ingawa biashara ya vinywaji vikali na mvinyo iliathiriwa kutokana na kupigwa marufuku kwa vifungashio vya plastiki maarufu kama viroba. Hata hivyo kampuni ilijipanga kwa haraka na kufanikiwa kukuza biashara za vinywaji hivyo katika kipindi kifupi kutokana na umaarufu na kukubalika kwa bidhaa zake katika soko.

6.3. Kampuni iliweza kubadilisha mwelekeo wa kushuka kwa mauzo kwa kutumia mkakati wa kutumia bidhaa zenye bei nafuu na zilizojazwa kwenye chupa ndogo uliowezesha wateja kumudu kununua bidhaa zake na kuwawezesha wengi wao kuacha kutumia pombe za kienyeji ambazo tafiti zinaonyesha kuwa zinatawaka soko kwa asilimia 50%, mkakati huu mbali na kuwezesha wateja kumudu kununua bidhaa zetu pia ulipunguza matumizi ya pombe haramu. Utendaji huu ulioleta mafanikio haya umedhihirisha jinsi kampuni ilivyo na uongozi madhubuti ambao una dhamira ya kufanikisha matarajio ya wanahisa wake.

6.4. Katika kipindi hiki, kampuni iliwekeza mtaji unaofikia shilingi 71,486 milioni kwa ajili ya kufanikisha ongezeko la mauzo ya bidhaa zake. Kwa niaba ya Bodi na Wanahisa, Mwenyekiti aliwapongeza wafanyakazi wa kampuni ambao jitihaza zao zimewezesha kupatikana mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi cha mwaka huo. Mwenyekiti pia aliwashukuru wateja, watumiaji wa bidhaa, wazabuni na wabia wa kibiashara kwa kuendelea kuiamini na kuiunga mkono kampuni. Bila wao isingewezekana kufanikisha ndoto ya kuwa kampuni bora barani Afrika, inayokua kwa kasi na kwa ufanisi mkubwa, inayovutia kila mtu kufanya nayo kazi, na ikiwa na dhamira ya kuleta mabadiliko katika jamii.

6.5. Mwenyekiti aliishukuru Serikali kwa jitihada inazofanya kuimarisha uchumi, ikiwa inatoa kipaumbele katika suala la kukuza sekta ya viwanda na kujenga mazingira mazuri ya biashara. Aliwashukuru pia wajumbe kwa uaminifu na mchango wao, ambao wamekuwa wakiutoa wenye lengo la kukuza biashara za kampuni. Aliwakaribisha wajumbe kuendelea

kutoa mawazo, kujadiliana na kuweka maazimio yenye lengo la kujenga kutokana na ajenda aambazo ziliwasilishwa mbele yao.

6.6. Akitoa ufafanuzi wa maoni yaliyotolewa na Wanahisa, Mkurugenzi Mkuu, alisema upigwaji marufuku wa vifungashio vya plastiki uliathiri biashara hasa za kampuni ya TDL. Iwapo kusingekuwa na katazo hilo, mauzo ya TDL yangekuwa mazuri zaidi kwani takribani asilia 70 ya bidhaa za kampuni hiyo zilikuwa zinatumia vifungashio hivyo. Kutokana na changamoto hiyo kampuni kwa haraka ilikuja na mkakati wa kutumia vifungashio vya chupa kwa kinywaji cha Konyagi ambacho kiliendelea kutamba katika soko la ndani na nje.I ngawa kinywaji cha Valuer ambacho kulikuwa kinapatikana kwa vifungashio vyenye ujazo wa ml 50 na ml 100 hakitengenezwi tena katika ujazo huo. Uongozi ulikuwa katika majadiliano na Serikali kuhusu ushuru wa kinywaji cha Valuer ambao uliathiri wakulima wa zao la Zabibu mkoani Dodoma.

6.7. Wajumbe walielezwa kuacha kuamini taarifa za uzushi zinazosambazwa zinazodai kuwa bei ya bia itashuka hadi kufikia shilingi 1,000/-. Bei ya bia ilishuka kwa wastani wa asilimia 10% kutokana na mabadiliko ya mkakati ambao uliwezesha kukuza mauzo katika mwaka uliopita. Kuingiza bidhaa zetu katika soko zikiwa katika vifungashio vidogo kwa lengo la kuwezesha wateja wetu kumudu kuzitumia ambapo chupa yenye ujazo wa ml 375 inauzwa kwa shilingi 1,500/- Uongozi utaendelea kushirikiana na Serikali ili kufanikisha mtazamo wetu wa kuongeza mauzo na kutoa mchango wa kuleta maendeleo kupitia kukusanya na kulipa kodi.

6.8. Wajumbe waliuliza ni mambo gani mazuri watarajie yatapatikana kutokana na mabadiliko katika uendeshaji wa shughuli za kampuni. Wajumbe walihakikishiwa kuwa ABInBev, ingeboresha zaidi mifumo ya uendeshaji sambamba na mifumo iliyokuwa inatumiwa na SABMiller. Baadhi ya mifumo ilishaanza kutumika na kuonyesha mafanikio kama vile katika kitengo cha ununuzi, uendeshaji wa viwanda, na usambazaji, Mifumo hii ilifanikisha kupunguza gharama za uendeshaji na kupunguza wafanyakazi wa kigeni kwenye kampuni. Mtazamo wa sasa ni kuwa na kampuni ya kisasa ambayo bidhaa zake zinatawala katika soko.

6.9. Katika mkakati wa kuendelea kufanya vizuri katika masoko, ilielezwa kuwa licha ya ushindani wa bei, kampuni ingeendelea kukabiliana nao kwa kutumia kila mbinu kama kutumia bidhaa zake zenye ubora wa hali ya juu na kutumia vifungashio vinavyokidhi matakwa ya wateja. Fursa kubwa iliyolengwa ni kuongeza watumiaji wa bidhaa zetu kwa kuwa soko la pombe za kienyeji bado ni kubwa.

6.10. Ufafanuzi kuhusu biashara ya mvinyo, wajumbe walielezwa kuwa bado kuna fursa kubwa katika biashara ya mvinyo nchini Tanzania na kwamba kampuni inabuni mkakati kuhakikisha inazalisha bidhaa za mvinyo kutokana na zabibu inayolimwa hapa nchini na kunufaika na nafuu ya kodi.

6.11. Wanachama walipitia na kuidhinisha Taarifa za fedha za mwaka na Taarifa za Wakurugenzi

KUMB.. NAMBA 7/2018 : KUTHIBITISHA NA KUPITISHA GAWIO KWA MWAKA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2017

7.1. Azimio la kuidhinisha malipo ya gawio la shilingi 770/- kwa kila hisa zilizolipwa katika kipindi kilichoishia Desemba 31, 2017 liliwakilishwa.

7.2. Wanahisa walilipokea na kuthibisha malipo ya gawio la shilingi 770/- kwa kila hisa katika kipindi kilichoishia tarehe 31, Desemba 2017.

KUMB.. NAMBA 8/2018: KUCHAGUA KAMPUNI YA UKAGUZI WA HESABU ZA BIASHARA

8.1. Wakurugenzi walipendekeza ichaguliwe kampuni ya PricewaterhouseCoopers ya Dar es Salaam, kuwa mkaguzi wa hesabu za kampuni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2018.

8.2. Wanahisa walipitisha uteuzi wa kampuni ya PricewaterhouseCoopers kama wakaguzi wa nje wa mahesabu ya kampuni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2018.

KUMB. NAMBA 9 /2018 : MENGINEYO

9.1. Kuhusiana na wazo la mwanahisa la kuanza usambazaji wa bia za mitungi katika miji mikubwa kama Dar es Salaam na kuingiza kinywaji cha Stella Artois katika soko la Tanzania, ilielezwa kuwa bia za mitungi tayari zinasambazwa na kuuza katika maeneo ya mijini na zoezi hilo lingeendelea kukua siku hadi siku. Changamoto ilikuwa gharama za kutunza vifaa vya kusambazia ambavyo vinahitaji kuwa katika usafi wa hali ya juu wakati wote.

9.2. Stella Artois, ni moja ya bidhaa maarufu ya ABInBev ambayo inafanya vizuri katika masoko mbalimbali duniani sambamba na bidhaa nyingine maarufu kama Corona na Budweiser. Budweiser tayari ilizinduliwa katika soko la Tanzania na inaendelea kukubalika kwa wateja wengi Jijini Dar es Salaam.

KUMB. NAMBA 10/2018 : KUFUNGA MKUTANO

10.1. Mwenyekiti aliwashukuru wanahisa kwa kuhudhuria, kwa mawazo yao mazuri waliyoyatoa na kuahidi kuwa yangefanyiwa kazi, ili kuongeza ufanisi katika utendaji wa kibiashara na kufanikisha mkakati wa ukuaji wa biashara za kampuni. Alisema mkakati ni kuendelea kutumia bidhaa zenye bei nafuu hivyo kuwezesha wateja kumudu kununua bidhaa za kampuni na kuendelea kutekeleza sera ya ununuzi wa malighafi ndani ya nchi.

10.2. Mwenyekiti alipongeza Uongozi wa kampuni kwa kufanikisha kupunguza matumizi katika uendeshaji, kwa kupunguza idadi ya wafanyakazi wa kigeni na kuwapatia fursa watanzania kushika nafasi mbalimbali za utendaji. Pia alisema anavutiwa na sera ya ABInBev ya kutoa fursa kwa vijana kuwa Mameneja wa vitengo ambayo inaenda sambamba na mtazamo wa nchi wa kutoa fursa kwa vijana.

10.3. Mwenyekiti alifunga mkutano saa sita na dakika 20 mchana

IMEPITISHWA: ----------

MWENYEKITI

TAREHE: ----------

WALIOHUDHURIA

1	ADELAIDE A. MUSHI	MJUMBE
2	ADRIAN S. MAKELELE	MJUMBE
3	ALDON MASHOBOZI	MJUMBE
4	AUGUSTINE A. MOSHI	MJUMBE
5	CHIEF MOSES CHALE	MJUMBE
6	CHILDREN CAREER PLAN	MJUMBE
7	CORE SECURITIES LTD	MJUMBE
8	DANIEL J. TIMOTHEO	MJUMBE
9	DAUNI E. IMIBONI	MJUMBE
10	DEOGRATIAS POLYCARP	MJUMBE
11	EDGER LUKANDA	MJUMBE
12	EDNA J. MBWANA	MJUMBE
13	EDWARD D. MIKINA	MJUMBE
14	EMANUEL S. KIBEYA	MJUMBE
15	EUPHRASIA GASPAR FUNDI	MJUMBE
16	FERDINAND S. SWAI	MJUMBE
17	FLORIDA R. KAZURA	MJUMBE
18	FRED ODATT	MJUMBE
19	GASPAR MICHAEL FUNDI	MJUMBE
20	GEORGE MUSSA	MJUMBE
21	GLOBAL MUSTER FUND	MJUMBE
22	H.E HON BARACK GHREE	MJUMBE
23	HARRISON SHIRIMA	MJUMBE
24	HUSSEIN M. KAPERA	MJUMBE
25	KENETH B. NGAILLAH	MJUMBE
26	MAGANGA M. SENGELEMA	MJUMBE
27	MATILDA RICHARD TEMBA	MJUMBE

28	MESHACK CHACHA	MJUMBE
29	MUHARAM MCHAME	MJUMBE
30	NAFTAL L. KISINGA	MJUMBE
31	NGAILLAH ELECTRICAL	MJUMBE
32	NSSF UGANDA	MJUMBE
33	ORBIT SECURITIES CO	MJUMBE
34	REGULAR INCOME TRUST	MJUMBE
35	ROBERT E MSANGI	MJUMBE
36	RUBAMBWA ABDON	MJUMBE
37	SIMON BABIA KATARAMA	MJUMBE
38	TANZANIA TOOTH HEALING	MJUMBE
39	UMOJA TRUST SCHEME	MJUMBE
40	UTT AMIS	MJUMBE
41	WILLIAM SHILA ELIAS	MJUMBE